TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)

TAARIFA KWA UMMA

MAAMUZI YA TUME YA VYUO VIKUU KUHUSU KUFUTA USAJILI WA KITUO KIMOJA CHA CHUO KIKUU, KUHAMISHA WANAFUNZI WANAOENDELEA NA MASOMO, NA KUSITISHA UDAHILI WA WANAFUNZI WAPYA KATIKA BAADHI YA VYUO VIKUU NCHINI

1.0 Utangulizi

Itakumbukwa kwamba mwaka 2016 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilifanya ukaguzi maalum wa kuhakiki ubora katika vyuo vya elimu ya juu nchini. Katika ukaguzi huo baadhi ya vyuo viligundulika kuwa na mapungufu kadhaa yanayoathiri utoaji wa elimu bora. Aidha, Tume iliendelea kuvishauri na kuelekeza vyuo kurekebisha mapungufu hayo kwa nyakati tofauti, sambamba na kufanya kaguzi za kawaida na za kushtukiza katika baadhi ya Vyuo Vikuu kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ili kujiridhisha kama maelekezo yametekelezwa na mapungufu yaliyobainishwa yamerekebishwa.

2.0 Maamuzi ya Tume

Kutokana na changamoto za ubora zilizobainishwa katika ukaguzi uliofanywa na Tume, na kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na wahitimu wenye kukidhi viwango bora vya elimu kitaifa na kimataifa kwa manufaa yao binafsi, jamii zao na Taifa kwa ujumla, Tume katika Kikao chake cha 84 kilichofanyika tarehe 25 Oktoba 2018 na kikao maalumu cha 85 kilichofanyika tarehe 7 Novemba 2018, imefanya maamuzi yafuatayo:

2.1. Kufuta usajili wa Kituo cha Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCo) na kuamuru Wanafunzi wote wanaoendelea na masomo wahamishwe

Tume imefuta usajili wa Kituo cha mjini Moshi cha Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCo – Town Centre) na kuamuru wanafunzi wote wanaoendelea na Masomo wahamishiwe katika Kampasi Kuu ya chuo hicho iliyopo Masoka, Moshi – Kilimanjaro.

2.2. Kuzuia udahili wa wanafunzi wapya na kuamuru kuhamishwa wanafunzi wa shahada ya kwanza wanaoendelea na masomo katika jumla ya programu tisa (9)

Tume imezuia udahili wa wanafunzi wapya na kuamuru kuhamishwa mara moja wanafunzi wa shahada ya kwanza wanaoendelea na masomo kwa mwaka 2018/19 katika jumla ya programu tisa (9) za shahada ya kwanza kutoka Vyuo Vikuu vinne (4) kama ifuatavyo:

a) Wanafunzi wote wanaosoma programu zifuatazo za Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia (IMTU), Dar es Salam.
   i) Bachelor of Medicine and Bachelor of Surgery (MBBS); na
   ii) Bachelor of Science in Nursing (BSc.N.)

b) Wanafunzi wote wanaosoma programu ya udaktari wa binadamu (Doctor of Medicine (MD)) ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu James (AJUCo), Songea – Ruvuma.

c) Wanafunzi wote wanaosoma programu zifuatazo za Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCo), Moshi – Kilimanjaro.
   i) Bachelor of Arts in Mass Communication; na
   ii) Bachelor of Arts in Public Administration and Management.

d) Wanafunzi wote wanaosoma programu zifuatazo za Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU), Lushoto - Tanga
   i) Bachelor of Education Special Needs (Arts);
   ii) Bachelor of Education Special Needs (Science);
   iii) Bachelor of Science with Education; na
   iv) Bachelor of Laws.

e) Aidha Tume imeridhia ombi la Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi (SMMUCo), Moshi – Kilimanjaro kuhamisha wanafunzi wa programu zifuatazo:-
   i) Certificate in Hospitality and Tourism Studies
   ii) Diploma in Mass Communication
   iii) Certificate in Mass Communication

2.3. Kuendelea kusitisha udahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu viwili (2)

Tume imeendelea kusitisha udahili wa wanafunzi wapya kwa ngazi zote za masomo katika Vyuo Vikuu vifuatavyo:

a) Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mt. Fransisko (SFUCHAS), Ifakara - Morogoro; na

b) Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo Tabora (AMUCTA), Tabora.

Kusitishwa udahili wa wanafunzi wapya katika vyuo hivi kunafanya jumla ya vyuo vikuu vilivyositishwa udahili kwa mwaka wa masomo 2018/19 kufikia kumi na mbili (12). Vyuo hivi vitaendelea kuwa chini ya uangalizi maalum wa Tume, vitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wengine wanaoendelea na masomo na haviruhusiwi kudahili wanafunzi wapya kwa ngazi zote za masomo (kuanzia astashahada, stashahada, shahada, shahada ya uzamili, hadi Shahada ya Uzamivu) kwenye programu zote za masomo mpaka hapo itakapoamriwa vinginevyo. Wanafunzi waliohitimu masomo kwa mwaka 2017/18 watatunukiwa tuzo (awards) zao katika vyuo walivyosoma.

3.0 Maelekezo Mahsusi

1. Tume inavitaka Vyuo Vikuu Vyote vilivyotajwa katika taarifa hii kuzingatia na kutekeleza maelekezo haya mara moja.
2. Vyuo Vikuu vyote vinavyotakiwa kuhamisha wanafunzi vinaagizwa kufuata taratibu za uhamisho na kukamilisha zoezi la uhamisho wa wanafunzi ndani ya wiki mbili (2) kuanzia tarehe 7 Novemba 2018.
3. Tume inaviagiza Vyuo Vikuu vyote ambavyo wanafunzi wao wanatakiwa kuhama kuwasiliana haraka na vyuo wanavyotakiwa kuhamia na kuwasilisha taarifa zote za wanafunzi kwa vyuo wanavyohamia.
4. Tume inaviagiza vyuo vyote vilivyoelekezwa kuhamisha wanafunzi, kuwaarifu mara moja wanafunzi wote kuhusu vyuo wanavyotakiwa kuhamia kama walivyoelekezwa.

4.0 Hitimisho

Tume haitasita kuchukua hatua stahiki kwa chuo chochote ambacho kitakiuka sheria na miongozo ya uthibiti ubora kwa kisingizio cha aina yoyote.

Imetolewa na

KATIBU MTENDAJI
09/11/2018